UNITED NATIONS CONFERENCE ON TRADE AND DEVELOPMENT
UNCTAD

# INFORMATION NOTE

**EMBARGO**

Yaliyomo ya kutolewa kwa waandishi wa habari hii na ripoti inayohusiana haipaswi kuchukuliwa au kwa muhtasari katika magazeti, matangazo au vyombo vya habari vya elektroniki kabla **ya Novemba 22, 2017, 5pm. GMT**

**(Saa 12 jioni, New York, 6 jioni, Geneva; 10.30 p.m., New Delhi, 2 asubuhi, 23 Novemba 2017, Tokyo)**

UNCTAD/PRESS/IN/2017/11*
*Original: English*

## LDC –RIPOTI YA NCHI MASKINI ZAIDI DUNIANI YA MWAKA 2017: UKWELI NA TAKWIMU

*Geneva, Uswisi, (22 Novemba 2017)*

### Tatizo

- Katika nchi maskini zaidi duniani (LDCs), watu milioni 577, au asilimia 62 ya watu, hawana huduma ya umeme.
- Katika watu wasio na huduma ya umeme duniani kote, asilimia 54 wanaishi katika nchi maskini zaidi duniani, mgawanyo ambao umeongezeka maradufu kutoka asilimia 30 mwaka 1990.
- Katika nchi maskini zaidi duniani, asilimia 82 ya watu wanaoishi katika maeneo ya vijijini hawana huduma ya umeme.
- Kufanikisha Lengo la Maendeleo Endelevu namba 7 ("Hakikisha upatikanaji wa nishati ya bei nafuu, inayoaminika, endelevu na ya kisasa kwa wote") kutatimiza wajibu muhimu katika kufikia Malengo mengine ya Maendeleo Endelevu, na mafanikio yake yataamua mafanikio au kushindwa kwa Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.
- Kufanikisha upatikanaji wa umeme kwa wote kufikia mwaka 2030 itahitaji ongezeko la asilimia 350 la idadi ya watu katika nchi maskini zaidi duniani wanaopata umeme kila mwaka, ikilinganishwa na muongo uliopita. Huu ni upanuzi mkubwa zaidi wa uzalishaji umeme kuliko katika kipindi cha 1990 – 2014, tena ndani ya muda mfupi zaidi.

### Changamoto

- Ingawa uzalishaji wa umeme katika nchi maskini zaidi duniani uliongezeka mara nne zaidi katika kipindi cha 1990 – 2014, huku ongezeko kubwa zaidi likiwa katika muongo uliopita, uzalishaji wa umeme kwa kila mwananchi uliongezeka kwa kiasi cha 2.5 kutokana na ongezeko la idadi ya watu.
- Uwezo wa uzalishaji umeshindwa kushika kasi huku kukiwa na ongezeko la asilimia 460 la idadi ya watu wanaopata umeme tangu mwaka 1991. Ilipofika 2014, msimiko wa uwezo wa kuzalisha umeme kwa kila mtu anayepata umeme haukufikia hata nusu ya kiwango cha mwaka 1991, wakati uzalishaji wa umeme kwa kila mtu anayepata umeme ulikuwa moja ya tano chini ya kiwango cha 1991.
- Watumiaji wa viwandani na biashara katika nchi maskini zaidi duniani, kwa wastani, hulipa mara mbili zaidi kwa ajili ya umeme kuliko wenzao katika nchi nyingine.

* **Contacts**: UNCTAD Communications and Information Unit, 41 22 917 58 28, 41 79 502 43 11, unctadpress@unctad.org, http://unctad.org/press.

To receive our press material, please register at http://unctad.org/en/Pages/RegisterJournalist.aspx.

- Miongoni mwa shughuli za kibiashara katika nchi maskini zaidi duniani, asilimia 42 hutoa taarifa kuwa wanakwamishwa na ukosefu wa upatikanaji wa nishati ya kutosha, inayoaminika na nafuu.
- Kwa wastani, makampuni katika nchi maskini zaidi duniani hupata matatizo ya umeme mara 10 kwa mwezi, ambayo hudumu kwa takribani saa tano, na hii hugharimu asilimia 7 ya thamani ya mauzo ya jumla.
- Kufikia kima cha chini cha mahitaji ya jamii ya kisasa katika nchi maskini zaidi duniani ungehitaji ongezeko la kiasi cha uzalishaji umeme cha 13.5 mwaka 2014
- Hata makadirio ya juu ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya nishati kila mwaka katika nchi maskini zaidi duniani, dola za Kimarekani bilioni 40, hayazingatii upatikanaji wa nishati iletayo mabadiliko.
- •Teknolojia mbadala kadhaa zimefaidika kufuatia punguzo kubwa la gharama, kutokana na ubunifu na mchakato wa kuongeza uzalishaji kwa njia ya elimu. Kwa mfano, gharama ya vifaa vya umeme wa jua imepungua kwa asilimia 85 katika muongo uliopita. Lakini bado gharama kubwa za awali na changamoto kuhusiana na uhamishaji na utohozi wa teknolojia inaashiria kuwa mafanikio haya huenda yasikamilike katika muktadha wa nchi maskini zaidi duniani.
- Nchi maskini zaidi duniani kwa kawaida huzalisha umeme kwa mchanganyiko wa njia mbili ambazo hutegemea mafuta na umeme wa maji
- Matumizi ya umeme usiotokana na maji kwenye uzalishaji uliounganishwa kwenye gridi huwa mdogo, chini ya asilimia 1.
- Chini ya asilimia 1 ya gesi itokanayo na mabaki ya mimea kwenye shamba kitalu (*greenhouse)* hutengenezwa kwenye nchi maskini zaidi duniani.
- Inakadiriwa kwamba kufikia upatikanaji wa nishati kwa wote mwaka 2030 itahitaji watu milioni 571 zaidi katika nchi maskini zaidi duniani wawe wameunganishwa kwenye gridi na zaidi ya watu milioni 341 kuunganishwa kwenye gridi ndogo; watu zaidi ya milioni 114 watahitaji mifumo ya kipekee isiyounganishwa.
- . Usambazaji wa gridi ndogo unapaswa kupanuliwa kwa kiasi kikubwa, ili kuhakikisha kwamba kiasi cha asilimia 35 ya watu katika nchi maskini zaidi duniani wanafikiwa na umeme.

**Ushirikiano wa kimataifa**

- Nusu ya mitambo ya kuzalisha umeme inayoingizwa katika nchi maskini zaidi duniani na asilimia 70 ya mitambo inayotumia umeme na vifaa hutoka katika nchi nyingine zinazoendelea.
- Katika mwaka 2015, asilimia 1.8 ya msaada rasmi wa maendeleo kwa nchi maskini zaidi duniani ilielekezwa kwenye sekta zao za nishati.
- Kutimiza malengo yaliyokubaliwa kimataifa kungeongeza mara nne msaada rasmi wa maendeleo kwa nchi maskini zaidi duniani.

Ripoti: http://unctad.org/en/pages/PublicationWebflyer.aspx?publicationid=1902
Video: unctad.org/ldcr2017/video

*** ** ***